

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

*Jarida Maalumu*

*No. 1*

# Yaliyojiri mwezi OKTOBA 2020





# Yaliyomo


1. Wafugaji watakiwa kutumia chanjo za Mifugo zinazotengenezwa na TVI.................................................. 1
2. Wafugaji washauriwa kutumia chakula bora kwa Mifugo yao.................................................................... 2
3. Maafisa Ugani wa Singida na Dodoma wapatiwa mafunzo rejea kuhusu ufugaji wenye tija............................. 3
4. KMM: Ogesheni Mifugo yenu ili kuikinga na magonjwa.......... 4
5. Watumishi watakiwa kuzifahamu sheria na taratibu za Utumishi wa Umma.................................................... 7
6. Dkt. Tamatamah akabidhi vipande vya kamba kwa wakulima wa mwani......................................................... 8
7. "Ukusanyaji wa Takwimu utasaidia kutoa tathmini ya hali ya Rasilimali za Bahari nchini" - Bulayi................................. 10
8. Kupunguza uvuvi haramu kwapandisha mapato ya Mkinga... 12
9. Sekta ya Uvuvi inatoa asilimia 30 ya Protini kwenye lishe - Dkt. Tamatamah....................................................... 13
10. Bilioni 4.2 zatumika kufufua Shirika la TAFICO........................ 14
11. Serikali yagawa injini za boti kwa vyama vya wavuvi Kanda ya Ziwa Victoria...................................................... 15

# WAFUGAJI WATAKIWA KUTUMIA CHANJO ZA MIFUGO ZINAZOTENGENEZWA NA TVI

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel amewataka wafugaji kutumia chanjo zinazozalishwa na Taasisi ya Chanjo Tanzania.

Prof. Gabriel aliyasema hayo wakati wa kikao na wahariri wa Vyombo vya habari kilichofanyika katika ofisi za taasisi hiyo Oktoba 3, 2020 kwa lengo la kuwaeleza shughuli mbalimbali zinazofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kuendeleza Sekta ya Mifugo hapa nchini.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kuhakikisha inadhibiti magonjwa ya mifugo, imeweka mikakati ya kutengeneza chanjo za magonjwa 13 ambapo katika magonjwa hayo tayari zimeshatengenezwa chanjo 6 zinazoendelea kutumika na wafugaji hapa nchini.

Wafugaji wametakiwa kuzitumia chanjo hizo zinazozalishwa na taasisi hiyo ya serikali kwani ni chanjo ambazo ubora wake umethibitishwa na taasisi za ubora.

Prof. Gabriel alisema lipo tatizo la baadhi ya wafugaji kutotumia wataalam wa mifugo katika maeneo waliyopo na hivyo kuzitumia chanjo hizo bila kupata ushauri wa wataalam hao. Hivyo aliwasihi wafugaji wote nchini kuhakikisha wanazitumia chanjo hizo baada ya kupata maelekezo kutoka kwa wataalam wa mifugo.

Uzalishaji wa chanjo hizo utasaidia nchi kuwa na usalama wa afya ya mifugo na hivyo kuwa na uhakika wa kuwa na afya njema ya wananchi wake. Zipo athari nyingi za kutozalisha chanjo hizo nchini kwani kwa kutegemea kununua chanjo kutoka nje ya nchi upo uwezekano wa adui kuidhuru mifugo na hatimaye kuzidhuru afya za wananchi.



**Meneja Taasisi ya Chanjo (TVI), Dkt. Stella Bitanyi (Kulia) akitoa maelezo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (aliyevaa suti) tarehe 03/10/2020 kabla hajaingia kwenye maabara na Wahariri wa Vyombo vya Habari ili waone kazi inayofanyika. Katikati ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari, Dkt. Furaha Mramba.**

Vilevile aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha wanatoa kipaumbele katika masuala ya chanjo za mifugo kama ambavyo zimewekwa kwa mujibu wa sheria kwamba asilimia 15 ya mapato ya ndani ya halmashauri yatumike kuendeleza sekta ya mifugo.

Prof. Gabriel pia aliwataka maafisa mifugo katika ngazi za mikoa, halmashauri, kata na vijiji kuhakikisha wanatoa huduma kwa wafugaji waliopo katika maeneo yao.

Aidha, Prof. Gabriel aliongeza kwa kuitaka Taasisi hiyo ya Chanjo kuhakikisha wanakamilisha utengenezaji wa chanjo 7 zilizobaki ili magonjwa yote 13 yaweze kudhibitiwa na hatimaye afya ya mifugo pamoja na mazao yake iweze kuwa bora. Pia aliwataka wajipange kuhakikisha wanazalisha chanjo nyingi ili waweze kuziuza hadi nje ya nchi.

Prof. Gabriel aliwashukuru wahariri wa vyombo vya habari kwa ushirikiano wanaoutoa kwa wizara ya mifugo na uvuvi katika utoaji habari mbalimbali za shughuli zinazofanywa na wizaara hiyo ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa wafugaji na wavuvi.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu – TVLA, Dkt. Furaha Mramba alisema chanjo zinazozalishwa na kituo hicho ni chanjo ya mdondo na chanjo za bakteria ambazo ni za aina tano. Dkt. Mramba alisema chanjo hizo zina ubora wa kimataifa kwani huwa zinapelekwa kuhakikiwa na taasisi za ubora.

Bw. Mgaya Kingoba ambaye ni mhariri kutoka gazeti la habari leo, alimshukuru Katibu Mkuu Gabriel kwa kuitisha kikao hicho ambacho kimewasaidia kupata uelewa wa mambo mbalimbali ya wizara hiyo ambayo yatawasaidia katika utekelezaji wa shughuli zao za kuhabari. Pia kwa niaba ya wahariri wenzake alimuahidi Katibu Mkuu kuwa wataendele kutoa ushirikiano kwa wizara hiyo.

# WAFUGAJI WASHAURIWA KUTUMIA CHAKULA BORA KWA MIFUGO YAO

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel amewataka wafugaji kote nchini kuacha tabia ya kuwapa mifugo yao vyakula ambavyo havijakaguliwa na wakaguzi wanaotambulika na Wizara hiyo kwani vyakula hivyo kwa kiasi kikubwa vinaleta magonjwa kwa mifugo.

Prof. Gabriel aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo kwa Wakaguzi wa chakula cha mifugo kutoka katika Mikoa ya Kanda ya Mashariki yaliyofanyika Mkoani Morogoro Oktoba 23, 2020.

Akiongea na Wakaguzi hao, Prof. Gabriel alitumia nafasi hiyo kuwataka wafugaji kutumia chakula kinachozalishwa katika viwanda vinavyotambulika na serikali, huku akisema vyakula vinavyozalishwa mitaani vingi vinakosa ubora unaohitajika kwa matumizi ya mifugo.

Aidha, Prof. Gabriel alitumia nafasi hiyo pia kuziagiza taasisi zote zinazozalisha chakula cha mifugo hapa nchini kufanya tafiti za kina katika malighafi zote zinazotumika katika kuchata chakula kama zinakidhi vigezo vya kutumika kama chakula cha mifugo.

Naye, Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo, Dk. Asimwe Rwiguza aliwataka wafugaji kuacha tabia ya kuwapa mifugo chakula ambacho hakifai kwa matumizi ya binadamu huku akisema kuwa chakula kisichofaa kwa binadamu pia hakifai kwa mifugo.

“Nyinyi kama Wataalam tumieni fursa hii ya mafunzo mliyoipata kwenda kutoa elimu kwa wafugaji juu ya namna bora ya kufuga kwa kuzingatia ufugaji wa kisasa” alisema Dkt. Asimwe.

Wakaguzi hao kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Pwani na Dodoma walipata fursa ya kutembelea Kiwanda kinachozalisha chakula cha mifugo cha ***International Tanfeeds*** kilichopo Mkoani Morogoro kwa lengo la kujifunza na kujionea hali ya uzalishaji kiwandani hapo.



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (kulia) akimvisha kitambulisho mmoja wa washiriki wa mafunzo ya ukaguzi wa vyakula vya mifugo ikiwa ni alama ya utambulisho wake kama mtaalam wa kukagua vyakula vya mifugo nchini katika mafunzo yaliyofanyika Mkoani Morogoro Oktoba 23, 2020.**

# MAAFISA UGANI WA SINGIDA NA DODOMA WAPATIWA MAFUNZO REJEA KUHUSU UFUGAJI WENYE TIJA

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani kutoka mikoa ya Singida na Dodoma ili kuwawezesha wagani hao kwenda kutoa elimu kwa wafugaji.

Akifungua mafunzo hayo Oktoba 7, 2020 Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani, Dkt. Angello Mwilawa alisema, wizara imekua ikitekeleza mikakati muhimu katika sekta ya mifugo ili kuweza kumsaidia mfugaji kufuga kisasa na kibiashara.

Mikakati hiyo ni pamoja na Uboreshaji wa Koosafu za mifugo nchini, Udhibiti wa magonjwa, Upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji katika maeneo yaliyo na mifugo, Kuboresha uzalishaji ulio wa kibiashara na ustawishaji wa ndege wafugwao, Kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ya ardhi, Kuhamasisha na kuanzisha vyama vya ushirika vya wafugaji na Kudhibiti upotevu wa mapato yatokanayo na mifugo pamoja na mazao yake.

Dkt. Mwilawa alisema katika kutekeleza mikakati hiyo wizara imekuwa ikipata changamoto nyingi ambazo ni ukosefu wa maarifa kwa wafugaji na ndio maana wizara imeamua kutoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani ili waweze kwenda kuwaelimisha wafugaji walioko katika mikoa yao.

Katika kutekeleza mikakati hiyo maafisa ugani wametakiwa kwenda kushirikiana na sekta na wadau wengine waliopo katika maeneo yao ili kuhakikisha wafugaji wanapata elimu hii na kuweza kufuga kwa tija.

Naye mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo na Mshauri wa mifugo kutoka sekretarieti ya mkoa



**Mkurugenzi wa Idara ya Utatifi, Mafunzo na Huduma Ugani, Dkt. Angello Mwilawa (aliyesimama) akionyesha kitini chenye mada za mafunzo rejea kwa maafisa Ugani na wafugaji Nchini wakati akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), yaliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Mipango Jijini Dodoma tarehe 7/10/2020.**

wa Singida, Dkt. David Mluma aliishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kutoa mafunzo rejea kwa kuwapatia ujuzi katika sekta ya mifugo.

Dkt. Mluma alisema mafunzo haya yamekuja muda mzuri kwani serikali kwa sasa inaendelea kuhamasisha wafugaji kuboresha koosafu za mifugo ili wafugaji waweze kuzalisha kwa tija. Lakini pia wamekumbushwa suala la udhibiti wa magonjwa ambalo usimamizi wake unasaidia mazao ya mifugo kuuzwa ndani na nje ya nchi.

Naye Afisa Mifugo kutoka Halmashauri ya Kondoa Mji, Semeni Mwakasege alisema mafunzo haya yamemsaidia kutambua sheria mbalimbali ambazo hapo awali hakudhani kama zinawahusu, hivyo ameahidi kwenda kuwaelimisha wataalamu wenzake pamoja na viongozi wa halmashauri ili wote kwa pamoja waweze kuzisimamia.

Pia ametoa wito kwa washiriki wenzake kuhakikisha kila mmoja anakwenda kutoa elimu waliyoipata kwa wataalam wenzao na wafugaji. Vilevile aliiomba wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuongeza wigo wa mafunzo haya ili wataalam wengi wa mifugo waweze kupata mafunzo haya ambayo yatasaidia kusambaza elimu hii kwa wafugaji wengi zaidi.

Mafunzo haya yametolewa kwa maafisa ugani 20 kutoka mikoa ya Singida na Dodoma na yamefanyika katika ukumbi wa chuo cha Mipango jijini Dodoma. Katika mafunzo hayo washiriki wameweza kupitishwa katika mada za Sheria Kanuni na Miongozo ya sekta ya mifugo, Udhibiti wa Magonjwa na matumizi ya dawa na viwatilifu, Sumukuvu, Madhara na namna ya kudhibiti, Mashamba darasa ya malisho na ustawishaji wa matunzo ya nyanda za malisho pamoja na uboreshaji wa koosafu za mifugo kwa ufugaji endelevu na tija.

# KMM: OGESHENI MIFUGO YENU ILI KUIKINGA NA MAGONJWA

Wafugaji hapa nchini wametakiwa kuogesha mifugo yao ili kuikinga na magonjwa yaenezwayo na kupe.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel Oktoba 10, 2020 wakati akizindua awamu ya tatu ya kampeni ya uogeshaji mifugo iliyofanyika katika Kijiji cha Bahi Sokoni, wilayani Bahi, mkoani Dodoma.

Prof. Gabriel alisema lengo kuu la kampeni hizo ni kuhamasisha wafugaji wote nchini kuunga mkono juhudi za serikali katika kuongeza tija ya ufugaji kwa kuwa na mifugo yenye afya njema, mifugo isiyo na magonjwa ambayo itazalisha mazao zaidi na yenye ubora wa kiwango cha kitaifa na kimatifa.

"Lengo la uogeshaji ni kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe hususani Ndigana kali (East Coast Fever – ECF), Ndigana Baridi (Anaplasmosis), Mkojo Mwekundu (Babesiosis) na Maji Moyo (Heart Water) ambayo yamekuwa yakiathiri mifugo na kusababisha hasara kubwa kwa mfugaji," alisema Prof. Gabriel.

Magonjwa yaenezwayo na kupe yasipodhibitiwa ipasavyo huchangia asilimia 72 ya vifo vyote vya ng'ombe hapa nchini. Kati ya magonjwa hayo, ugonjwa wa Ndigana Kali huchangia vifo kwa kiwango kikubwa cha asilimia 44. Hasara inayotokana na magonjwa yaenezwayo na kupe inakadiriwa kuwa ni dola za Marekani milioni 64.7 kwa mwaka sawa na takribani shilingi bilioni 145. Hasara nyingine ni pamoja na kupunguza uzalishaji wa maziwa, kupungua kwa nyama kutokana na kukonda, kushuka thamani ya Ngozi, kupoteza wanyamakazi na udumavu wa ndama.

Prof. Gabriel alisema serikali imenunua dawa za kuogesha mifugo aina ya Paranex, Paratop na Amitrax kiasi cha lita 15,579 zenye thamani ya shilingi 592,822,375 ambazo zinatosheleza majosho 1,983 katika halmashauri 162 na matarajio ni kifikia jumla ya



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (mwenye koti jeupe katikati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Kampeni ya Uogeshaji Mifugo Kitaifa awamu ya tatu katika kijiji cha Bahi Sokoni, wilayani Bahi, mkoani Dodoma tarehe 10/10/2020.**

michovyo 405,000,000 ya mifugo yote itakayoogeshwa.

Kupitia kampeni hizo, serikali imekuwa ikitoa dawa zenye ruzuku na bei elekezi za kuogeshea mifugo ambapo kwa ng'ombe ni shilingi 50, mbuzi na kondoo shilingi 10 kwa mchovyo mmoja ambapo wafugaji wengi wamehamasika kuogesha mifugo yao.

Pia serikali kuu, halmashauri na wadau wengine wamejenga majosho 101, kukarabati majosho 578 pamoja na kuunda kamati 1,036 zinazosimamia shughuli za uogeshaji wa mifugo katika majosho. Vilevile imeunda timu 12 ambazo huzunguka nchi nzima kwa ajili ya kuhamasisha shughuli za uogeshaji mifugo na ufuatiliaji wa miundombinu ya mifugo.

Katika kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, serikali imetunga Kanuni ya Uogeshaji na Matumizi ya Viuatilifu vya Mifugo (Acaricide Applications and Management Regulations, 2019). Kanuni hii inamlazimisha mfugaji kuogesha mifugo yake mara mbili kwa mwezi na serikali itasimamia zoezi la uogeshaji kwa ujumla.

Katika uzinduzi huo, Prof. Gabriel alitoa maelekezo kwa wafugaji wote nchini kuhakikisha wanaogesha mifugo yao ili kuikinga na magonjwa, halmashauri zote nchini kusimamia kanuni ya uogeshaji ili wafugaji waifuate maana majosho yapo na dawa zimeshatolewa, halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na wafugaji na wadau ziendelee kukarabati majosho yake na miundombinu mingine ya mifugo na halmashauri kuhamasisha wafugaji kuunda vikundi vitakavyosimamia uendeshaji endelevu wa majosho ikiwa ni pamoja na kufungua akaunti benki kwa ajili ya




**Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Dkt. Fatima Mganga (mwenye kilembe) akipokea madawa ya ruzuku ya kuogeshea Mifugo kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel kwa niaba ya wakurugenzi wa Halmashauri zote hapa nchini wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Uogeshaji Mifugo Kitaifa awamu ya tatu uliofanyika katika kijiji cha Bahi Sokoni, wilayani Bahi, mkoani Dodoma tarehe 10/10/2020.**

kuhifadhi fedha zinazokusanywa wakati wa uogeshaji mifugo.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Dkt. Fatuma Mganga alisema mifugo katika wilaya ya Bahi imekuwa ikichangia zaidi ya asilimia 55 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa mwaka. Lakini mifugo imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya magonjwa kama Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Ugonjwa wa Mapafu ya ng'ombe na mbuzi na kideri cha kuku. Halmashauri imekuwa ikidhibiti magonjwa haya kwa kuogesha na kunyunyizia mifugo viuatilifu, kutoa chanjo na kutoa ushauri wa kitaalam kupitia maafisa ugani waliopo katika kata na vijiji.

Nao wafugaji walioleta mifugo yao kwa ajili ya kuiogesha katika uzinduzi wa kampeni hiyo ya awamu ya tatu wilayani Bahi waliishukuru serikali kwa kufufua majosho na kujenga mengine mapya pamoja na kutoa ruzuku ya madawa ya kuogeshea mifugo kwani kwa kufanya hivyo wanaimani mifugo yao haitakufa tena kutokana na magonjwa yanayosababishwa na kupe.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga alisema kuwa awamu ya kwanza ya kampeni hii ilizinduliwa tarehe 16/12/2018 wilayani Chato na awamu ya pili uzinduzi wake ulifanyika tarehe 29/10/2019 katika halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi.

Prof. Nonga alisema katika kampeni ya awamu ya kwanza na ya pili serikali ilinunua jumla ya lita 21,373.06 za dawa zenye thamani ya 740,714,750 kwa lengo la kuhamasisha wananchi kuogesha mifugo yao. Katika awamu zote mbili kumekuwa na jumla ya michovyo 254,375,555 ya mifugo yote ikiwemo ng'ombe 176,320,815, mbuzi 58,012,461, kondoo 20,039,594 na punda 2,685.




**Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Mifugo (WMUV), Prof. Hezron Nonga akitoa taarifa fupi ya Kampeni ya Kitaifa ya Uogeshaji Mifugo hapa nchini kwa mgeni rasmi wakati wa uzinduzi wa awamu ya tatu ya Kampeni hiyo uliofanyika katika kijiji cha Bahi Sokoni, wilayani Bahi, mkoani Dodoma tarehe 10/10/2020.**

# WATUMISHI WATAKIWA KUZIFAHAMU SHERIA NA TARATIBU ZA UTUMISHI WA UMMA

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Bw. Zachariyya Kera amewataka watumishi wa umma kujijengea tabia ya kusoma katiba na sheria za kiutumishi ili kuzifahamu sheria na haki zao za msingi.

Akiongea wakati alipotembelea ofisi za Taasisi ya Chanjo za Mifugo Tanzania (TVI) Oktoba 20, 2020 zilizopo mkoani Pwani, akiambatana na baadhi ya viongozi waandamizi wa wizara hiyo sekta ya mifugo, Bw. Kera alitoa ufafanuzi wa mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwataka wafanyakazi kujua haki zao za msingi na kufuatilia kwa wakati.

“Watumishi waelimishwe kuhusu haki zao na wapate stahiki zao kwa wakati na kujijengea tabia ya kusoma sheria na taratibu za kiutumishi ili wasipitwe na mambo mengi.” alisema Bw. Kera.

Katika ziara hiyo ya baadhi ya viongozi waandamizi wa Wizara ya Mifugo na uvuvi sekta ya mifugo, walipata pia fursa ya kutembelea kituo cha uhimilishaji kanda ya mashariki (kibaha) kilichopo Mkoani humo na Shamba la Malisho Vikuge kujifunza shughuli mbalimbali zinazofanywa na kituo pamoja na shamba hilo.

Meneja wa Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI), Dkt. Stella Bitanyi alisema chanjo ni muhimu sana kwa mifugo kwani huboresha afya za mifugo na mfugo ukiwa na afya nzuri hata afya ya binadamu huimarika pale atumiapo, chanjo zinaongeza pato la taifa kwani huzalishwa na kuuzwa.

Aidha, Dkt. Bitanyi alitumia nafasi hiyo kuwaeleza watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi changamoto zinazowakabili ikiwa ni pamoja na upungufu wa vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi kwani wanatumia teknolojia ya chini sana katika utendaji wao wa kazi.

Hata hivyo ameshauri kuwe na utaratibu wa kutoa elimu kwa wataalam ya namna ya kutumia Chanjo kwani wengi hukosea na kuchanja maeneo yasiyostahili.

“Elimu ya uchanjaji inahitajika kwa wingi kwa wataalam wetu kwani wanachanja shingoni badala ya kuchanja nyuma ya kwapa kwenye ngozi.” Alisisitiza Dkt. Stella.

Mkuu wa kituo cha uhimilishaji kanda ya Mashariki (Kibaha), Bw. Anzigary Kasanga Balaka alieleza kazi wanazofanya ikiwa ni pamoja na kuzalisha mbegu bora za madume na kuuza, kutoa ushauri kwa wafugaji na kuboresha mifugo yao kwa uhimilishaji, kuratibu Mafunzo ya uhimilishaji na kuuza vitendea kazi vya uhimilishaji kama mitungi ya gesi.

Aidha, Viongozi wa TVI, Kituo cha Uhimilishaji na Shamba la Malisho Vikuge waliishukuru serikali ya awamu ya tano kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuendelea kuona umuhimu wa shughuli wanazofanya na kuwatembelea kujionea mazingira ya watumishi wao na changamoto wanazopitia katika maeneo yao ya kazi na kuzitafutia ufumbuzi.



**Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali-watu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bw. Zachariyya Kera (kulia) akitoa ufafanuzi wa utaratibu wa upandishwaji vyeo kwa watumishi wa Taasisi ya uzalishaji Chanjo za Mifugo Tanzania (TVI) walipotembelea kituo hicho Wilaya ya Kibaha, Mkoani Pwani tarehe 20/10/2020.**

# DKT. TAMATAMAH AKABIDHI VIPANDE VYA KAMBA KWA WAKULIMA WA MWANI

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah alikabidhi vipande vya kamba za manila 700,000 kwa wakulima wa mwani katika Kijiji cha Songosongo, wilayani Kilwa, mkoa wa Lindi.

Akizungumza na wananchi wa Songosongo Oktoba 19, 2020 Dkt. Tamatamah alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) imetoa kamba hizo ili kuwawezesha wakulima wa mwani kwani kamba ilikuwa ni mojawapo ya changamoto iliyokuwa ikiwakabili.

Kamba hizo za manila ambazo kila moja ina urefu wa mita 10 hufungwa katika vigingi na hutumika kwa ajili ya kuoteshea mwani ambapo mwani hufungwa katika kamba hizo ili kusaidia mwani kutochukuliwa na maji ya bahari pale panapokuwepo na mawimbi makali.

Dkt. Tamatamah alisema duniani kote kwa sasa mwani unalimwa kibiashara, hivyo mwani ni moja ya zao linalopewa kipaumbele katika wizara. Katika kilimo cha mwani wakulima wanakutana na changamoto mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa mitaji na masoko.

"Wizara kupitia sekta ya uvuvi imeanza kutoa kamba ambazo ni moja ya pembejeo muhimu kwa wakulima wa mwani ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha wakulima hao kwa kuwapunguzia sehemu ya gharama za uzalishaji ili baadae waweze kusimama wenyewe," alisema Dkt. Tamatamah.

Pia aliongeza kuwa kama wakulima watalima vizuri katika kamba moja ya mita kumi katika bamvua nne (miezi miwili) wanaweza kupata kati ya kilo 8-10, na kamba hizo walizopewa zinaweza kutumika kwa mwaka mzima. Lengo la wizara ni kusambaza kamba hizo kwa wakulima wa mwani maeneo yote Tanzania Bara. ▼



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (kulia) akimkabidhi Mwenyekiti wa kijiji cha Songosongo wilayani Kilwa, Bw. Swaluya Sadi (kushoto), kamba 700,000 kwa ajili ya wakulima wa mwani wilayani Kilwa tarehe 19/10/2020. Katikati ni Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dkt. Nazael Madalla.**



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah akizungumza na waandishi wa habari akiwa na baadhi ya wakulima wa mwani kwenye moja ya shamba la mwani alilolitembelea wakati wa ziara yake kwenye kijiji cha Songosongo, wilayani Kilwa kwa ajili ya zoezi la ugawaji kamba 700,000 kwa wakulima hao tarehe 19/10/2020.**

Dkt. Tamatamah alisema kuwa ipo changamoto ya soko la mwani hasa kwenye bei kwani kwa sasa asilimia 90 ya mwani inauzwa nje ikiwa ghafi na ni asilimia 10 tu ndio inayotumika hapa nchini.

Hivyo wizara kwa sasa inawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na kuwaunganisha na taasisi za fedha ili waweze kukopesheka na waweze kuanzisha viwanda vidogo vya kuchakata mwani ili kuuongezea thamani. Hii itasaidia kupunguza kiasi cha asilimia ya mwani inayokwenda nje ya nchi ikiwa ghafi na kusaidia kuongeza ajira.

Aidha, Katibu Mkuu Tamatamah alisema zao la mwani lina faida kubwa ikiwa ni pamoja na kuongeza kipato katika jamii za maeneo ya pwani hasa kwa akina mama, inaondoa umaskini lakini pia kuingiza fedha za kigeni.

Naye mkulima wa mwani, Bi. Mbimbisa Omary alimshukuru Katibu Mkuu Tamatamah kwa kuwaletea vitendea kazi kwa ajili ya kilimo cha mwani. Bi. Mbimbisa alisema kilimo cha mwani huwasaidia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuwasomesha watoto, kununua chakula pamoja na ujenzi wa nyumba.

Bi. Jaka Farahani ambaye ni mkulima wa mwani alisema changamoto ya masoko inawasumbua sana hasa pale wanunuzi wanaowategemea wasiponunua, hivyo ameiomba wizara kuwasaidia kutatua changamoto hiyo. Lakini pia amemuomba Katibu Mkuu kuendelea kuwapelekea kamba nyingi zaidi kwa kuwa eneo la kulima ni kubwa na wakulima wapo wengi.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dkt. Nazael Madalla alisema wizara kupitia idara yake inaendelea kuhamasisha kampuni kuendelea kuchukua leseni kwa ajili ya kununua mwani na mpaka sasa zipo kampuni 7. Lengo la kuwa na kampuni nyingi ni kuongeza ushindani hivyo kampuni zinahamasishwa kujisajili ili zitambulike na ziweze kufanya biashara ya mwani.

Zao la mwani hapa nchini Tanzania lilianza kulimwa miaka ya 1980 na lilianzishwa katika kisiwa cha Zanzibar. Baada ya kufanikiwa katika kipindi cha majaribio, miaka ya 1990 mpaka 2000 Tanzania hususani Zanzibar ilikuwa ni nchi ya kwanza duniani kwa uzalishaji wa mwani. Lakini kutokana na changamoto mbalimbali kwa sasa Tanzania ni nchi ya tatu kwa uzalishaji wa mwani ambapo nchi ya kwanza ni Ufilipino ikifuatiwa na Indonesia.

# "UKUSANYAJI WA TAKWIMU UTASAIDIA KUTOA TATHIMINI YA HALI YA RASILIMALI ZA BAHARI NCHINI" - Bulayi

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesema ukusanyaji wa takwimu za sekta ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi unalenga kutoa tathmini ya hali ya uvuvi katika ukanda huo na kuhakikisha rasilimali za bahari zinaendelea kuleta manufaa na kuchangia katika uchumi wa nchi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam Oktoba 09, 2020 wakati wa kufunga mafunzo ya siku mbili ya ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani yanayohusisha maafisa uvuvi na viongozi kutoka Vikundi vya Kusimamia Rasilimali ya Uvuvi Mwaloni (BMU), kutoka Mikoa ya Dar es Salaam katika Wilaya za Kinondoni, Kigamboni na Ilala pamoja na Mkoa wa Pwani ukihusisha Wilaya za Bagamoyo na Chalinze, Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi Bw. Emmanuel Bulayi alisema maendeleo ya wananchi katika eneo hilo yanategemea sana shughuli za uvuvi.

"Kwa hiyo suala la kuchukua takwimu na kujua rasilimali ikoje kila wakati na kila muda ni suala la msingi sana ni ukweli ulio wazi maendeleo ya wananchi katika hili eneo yanategemea sana shughuli za uvuvi, hivyo ni muhimu sana halmashauri na wananchi wanakuwa katika mstari wa mbele katika kuhakikisha tunaendelea na uchumi endelevu katika Ukanda wa Pwani kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo." alibainisha Bw. Bulayi

Aidha, amesema taarifa zinazochukuliwa wakati wa kukusanya takwimu kwa njia ya mfumo wa kieletroniki ni pamoja na kufahamu kiwango cha samaki wanaovuliwa kwa kilo, kwa boti na kwa siku, ni suala la msingi ili baadae serikali iweze kufahamu kiasi gani cha samaki kinachovuliwa na kuweka mipango itakayosaidia mikakati mbalimbali ya maendeleo.

Pia, Bw. Bulayi aliwataka wakusanya takwimu kuhakikisha wanakusanya takwimu halisia kwani bila kuzingatia hilo watalidanganya taifa, hivyo wanapaswa wafahamu jukumu kubwa walilonalo kwa ajili ya kuitumikia sekta ya uvuvi nchini.

"Takwimu ndio hasa tunasema ni msingi wa sekta ya uvuvi katika kuhakikisha wavuvi wanaendelea, lakini pia sekta inaendelea, lakini pia sekta tunanufaika nayo kwa hiyo bila takwimu hakuna la kuongea." alifafanua Bw. Bulayi

Mkurugenzi huyo wa Idara ya Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bw. Emmanuel Bulayi, aliwakumbusha pia washiriki wa mafunzo ya siku mbili ya ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani kuwa, ukusanyaji wa takwimu ya sekta ya uvuvi ni takwa la kidunia kupitia Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), lakini pia ni takwa la nchi hivyo washiriki wa mafunzo hayo wana jukumu kubwa katika ukusanyaji wa takwimu sahihi.

Alisema, mafunzo ya namna hiyo yanatarajia pia kuendelea kwenye halmashauri 15 katika Ukanda wa Bahari ya Hindi, hivyo kutaka uwepo ushirikiano wa kutosha kati ya maafisa uvuvi na wadau wa sekta ya uvuvi ili kuhakikisha rasilimali za bahari zinalinufaisha taifa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa



**Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bw. Emmanuel Bulayi na Mkurugenzi wa Uratibu wa Sekta kutoka Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Yusuf Semuguruka wakikabidhi vifaa vya kukusanyia takwimu kwa washiriki zikiwemo simu za mkononi, mizani, makoti ya mvua na mabuti tarehe 09/10/2020.**

Uratibu wa Sekta kutoka Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Yusuf Semuguruka, aliipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuandaa mafunzo hayo kwa kuwa serikali inaangalia uwepo wa Vikundi vya Kusimamia Rasilimali ya Uvuvi Mwaloni (BMU) katika kusaidia kutafuta taarifa sahihi kwa ajili ya maandalizi ya sera mbalimbali.

Bw. Semuguruka alisema TAMISEMI itafuatilia kuangalia mafunzo hayo namna yanavyowasaidia maafisa uvuvi na viongozi wa BMU katika kukusanya takwimu sahihi.

Kwa upande wao baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo ambao wamekuwa wakituma taarifa za takwimu kwa kutumia mfumo maalum wa njia ya simu ya mkononi katika ofisi za makao makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), wakizungumza kabla ya kuahirishwa kwa mafunzo hayo wakiwa kwenye mwalo wa samaki katika soko la Kunduchi jijini Dar es salaam walisema wamenufaika na mafunzo hayo yakiwemo ya namna ya kupata takwimu kwa usahihi.

Mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani yamefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga na baadaye yatafanyika katika Mkoa wa Mtwara kwa maafisa uvuvi na Vikundi vya Kusimamia Rasilimali ya Uvuvi Mwaloni (BMU), ambao wamekuwa wakikusanya takwimu hizo.

Mafunzo hayo yamehusisha ukusanyaji wa takwimu kwa kutumia sampuli za wingi wa samaki, idadi ya uchaguzi wa aina ya vyombo na zana za uvuvi, njia za ukusanyaji takwimu ikiwemo ya kutumia mfumo wa simu ya mkononi, namna ya kupata wastani wa uzito wa samaki pamoja na kufahamishwa umuhimu wa takwimu za uvuvi nchini.



**Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani wakipima uzito wa samaki kama sehemu ya mafunzo waliyopata, wakati walipotembelea soko la samaki katika mwalo wa Kunduchi jijini Dar es Salaam tarehe 09/10/2020.**

Washiriki wa mafunzo hayo wamepatiwa vifaa mbalimbali vya kukusanyia takwimu katika maeneo ya kazi zikiwemo simu za mkononi, mizani, makoti ya mvua na mabuti.

Mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani yaliandaliwa kupitia mradi wa usimamizi wa samaki wanaopatikana katika tabaka la maji la juu na kati unaotekelezwa kwa ushirikiano na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO).



**Picha ya pamoja ya washiriki wa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya uvuvi katika Ukanda wa Pwani wakiwa na baadhi ya maafisa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, mara baada ya kumaliza masomo ya vitendo katika mwalo wa Kunduchi jijini Dar es Salaam tarehe 09/10/2020.**

# KUPUNGUA UVUVI HARAMU KWAPANDISHA MAPATO YA MKINGA

Mapato ya Halmashauri ya Mkinga, Mkoani Tanga kupitia Sekta ya Uvuvi yamepanda kufikia shilingi Milioni 96.6 mwaka 2019/2020 kufuatia mikakati waliyoiweka dhidi ya Uvuvi haramu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga, Rashid Gembe alisema hayo wakati akiongea na timu ya Wataalamu kutoka Mradi wa Ulinzi Shirikishi wa rasilimali za bahari kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (SWIOfish) ofisini kwake Oktoba 1, 2020. Alisema kuwa kabla ya mradi huo kuanza kuhamasisha uvuvi endelevu na wenye tija, mwaka 2015/ 2016 Halmashauri ya Mkinga ilikusanya kiasi cha shilingi Milioni 45.3 kutoka katika sekta ya Uvuvi.

Gembe aliwaeleza wataalamu hao waliokwenda kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo Wilayani humo kuwa mradi umechangia kwa kiasi kikubwa kukomeshwa kwa uvuvi haramu hususani uvuvi wa kutumia mabomu na makokoro.

“Mradi wa SWIOfish ulipoanza kufanya kazi hapa Wilayani kwetu mwaka 2016 ulianzisha Vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Bahari (BMU) zipatazo 14 ambazo zimesaidia kutoa elimu ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa wananchi ikiwemo kutunza mazingira ya fukwe za bahari”, alisema Gembe

“Pamoja na kuimarisha BMU hizo, pia iliimarisha Doria za Baharini na nchi kavu kwa lengo la kulinda rasilimali za uvuvi, na nikiri kuwa Doria hizo zimesaidia kupungua kwa uvuvi haramu na sasa mapato ya Halmashauri yameanza kupanda kwa sababu wavuvi sasa wanafanya uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi”, aliongeza Gembe



**Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga, Rashid Gembe akieleza jambo wakati akitoa taarifa ya Utekelezaji wa Mradi wa Ulinzi Shirikishi wa rasilimali za bahari kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (SWIOfish) Wilayani Pangani Mkoani Tanga Oktoba 1, 2020.**

Kufuatia mafanikio hayo, Gembe aliuomba mradi wa SWIOfish kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi katika mwambao wa bahari wilayani humo ili rasilimali za uvuvi zilizopo ziendelee kuwanufaisha waliopo na vizazi vijavyo.

Aidha, aliwasihi wananchi wanaoishi katika mwambao wa bahari waliopata elimu hiyo ya utunzaji wa rasilimali za bahari na uoto wake kuendelea kuienzi elimu hiyo kwa kuisambaza kwa wengine ili rasilimali hizo ziendelee kunufaisha jamii hizo na Taifa kwa ujumla.

“Niwatake wananchi kuacha kukata mikoko na kuendelea kuwa sehemu ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi ili ziendelee kuwa na tija kwa jamii”, alisisitiza.

Aliwakumbusha wananchi wa Wilaya hiyo kuwa mapambano dhidi ya uvuvi haramu sio nguvu ya soda ni mapambano endelevu na hawatakuwa na huruma na yeyote atakaye kwenda kinyume.

“Wananchi watambue kuwa tunafanya haya kwa nia njema, sisi tutaondoka lakini hii nchi itaendelea kuwepo, tufikirie Tanzania ya miaka 50 ijayo, tusiwe na mawazo ya kupata sasa tu, huo utakuwa ubinafsi”, alifafanua Gembe.

Mkurugenzi huyo aliushukuru mradi wa SWIOfish kwa kuwapatia vifaa mbalimbali ambavyo vimeweza kuisaidia halmashauri hiyo kuvitumia katika kulinda rasilimali za bahari.

# SEKTA YA UVUVI INATOA ASILIMIA 30 YA PROTINI KWENYE LISHE- DKT. TAMATAMAH

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah amewataka wafugaji na wavuvi nchini kuacha kufanya kazi zao kwa mazoea na badala yake watumie njia za kisasa na kitaalam katika utekelezaji wa shughuli hizo.

Dkt. Tamatamah aliyasema hayo alipokuwa akiwasilisha taarifa za Sekta za Mifugo na Uvuvi wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Chakula duniani uliofanyika tarehe 10.10.2020 mkoani Njombe.

Katika taarifa yake Dkt. Tamatamah alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatambua umuhimu wa lishe bora kwa wananchi hususan wazee na watoto hasa kwa kuzingatia ukweli kuwa nyama na samaki ni vyakula vinavyotoa protini kwa wingi zaidi ukilinganisha na vyakula vingine.

"Mhe. Mgeni rasmi sekta ya uvuvi inachangia asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama huku ikichangia ajira kwa Watanzania takribani Milioni 4.5 katika shughuli mbalimbali za sekta hiyo" Alisema Dkt.Tamatamah.

Aidha aliongeza kuwa uzalishaji wa samaki kwa upande wa maji ya asili umefikia kiasi cha takribani tani 497,567 huku kwa upande wa uzalishaji viumbe maji ukifikia kiasi cha takribani tani 18,716.36.

Kwa upande wa Mifugo Dkt. Tamatamah alisema kuwa sekta hiyo imechangia ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia lishe bora, ajira, kipato cha mtu mmoja mmoja na fedha za kigeni ambapo kwa mwaka 2019/20 ilichangia pato la taifa kwa asilimia 7.4 na kukua kwa asilimia 5 ikilinganishwa na asilimia 4.9 kwa mwaka 2018/19.

"Nihitimishe taarifa yangu kwa kutoa rai kwa wananchi kuongeza ulaji wa bidhaa zitokanazo na mifugo na uvuvi ili kufikia kiwango kilichosimikwa na shirika la chakula la duniani (FAO)" Alimalizia Dkt. Tamatamah.



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah (kulia) akifafanua jambo kwenye banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya Mgeni rasmi ambaye pia Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Omary Mgumba (kushoto) wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Chakula duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Njombe tarehe 10.10.2020.**



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Prof. Elisante Ole Gabriel (kulia) akionesha samaki aina ya Jodari kwa Mgeni rasmi wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Chakula duniani ambaye pia ni Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Hasunga (kushoto) baada ya Mhe. Hasunga kufika kwenye banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) kwenye Viwanja vya Mji Mwema mkoani Njombe tarehe 16/10/2020.**

# BILIONI 4.2 KUTUMIKA KUFUFUA TAFICO

Serikali ya Japan imekubali kutoa msaada wa Yen Milioni 200 kwa ajili ya kusaidia ufufuaji wa shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO).

Haya yalibainishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi, Bw. Emmanuel Bulayi kwa niaba ya Katibu Mkuu Sekta ya Uvuvi, wakati akifungua kikao cha kujadili vigezo mbalimbali vitakavyowezesha kupatikana mapendekezo ya aina ya vifaa vya uvuvi vya TAFICO vitakavyonunuliwa kupitia ufadhili wa Japan, jijini Dar es Salaam Oktoba 1, 2020.

Bw. Bulayi alisema kuwa serikali inaendelea na mchakato wa ufufuaji wa shirika lake la TAFICO ambapo imepata msaada wa Yen Milioni 200 takriban shilingi za kitanzania Bilioni 4.2 kutoka serikali ya Japan kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii.

Fedha hizo zitatumika kununulia meli moja ya uvuvi, majokofu ya kuhifadhi samaki na mitambo ya kuzalisha barafu. Serikali ya Japan itanunua, itasafirisha, itasimika mitambo katika eneo la Ras Mkwavi, pamoja na kufundisha matumizi sahihi ya mitambo hiyo.

Bw. Bulayi aliwaeleza wadau wa kikao hicho kuwa serikali imeona ni vema wakashirikishwa ili na wao waweze kutoa ushauri kutokana na uzoefu walionao ili vifaa hivyo vitakapoagizwa viweze kukidhi mahitaji kama ilivyokusudiwa. Hivyo, ni muhimu majadiliano hayo yatakapokamilika, orodha ya vifaa hivyo iweze kujulikana.

Naye Kaimu Meneja Mkuu TAFICO, Bi. Esther Mulyila alisema lengo la kikao hicho ni kujadili aina ya vifaa vya uvuvi vitakavyonunuliwa kwa ajili ya meli ya uvuvi, majokofu kwa ajili ya kuhifadhia samaki na mtambo wa kuzalishia barafu.

Bi. Mulyila aliongeza kuwa TAFICO kwa sasa itatekeleza majukumu yake pamoja na miradi 10 yenye thamani ya bilioni 89.8 itakayotekelezwa kwa awamu kwa kushirikisha wadau.

Miradi hiyo imegawanyika katika maeneo matatu, ambayo ni miradi ya uvuvi kwa kutumia meli za aina 3 za uvuvi, mradi wa mtambo wa kuzalisha barafu, mradi wa majokofu ya kuhifadhia samaki, mradi wa viwanda vya uchakataji samaki, miradi ya ukuzaji viumbe maji (uzalishaji wa vifaranga vya samaki, uzalishaji wa vyakula vya samaki, ufugaji wa samaki kwenye vizimba na ufugaji wa samaki kwenye mabwawa).

Kikao hicho cha wadau kilihusisha washiriki kutoka kampuni za uvuvi, TDB, THA, DMI, FETA, TAFIRI, TASAC, Menejimenti ya TAFICO, Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu na wawakilishi wa Idara ya Uvuvi.



**Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi, Bw. Emmanuel Bulayi akifungua kikao (kwa niaba ya Katibu Mkuu Uvuvi) cha kujadili vigezo mbalimbali vitakavyowezesha kupatikana mapendekezo ya aina ya vifaa vya uvuvi vya TAFICO vitakavyonunuliwa kupitia ufadhili wa serikali ya Japan. Kulia kwake ni Kaimu Meneja Mkuu TAFICO, Bi. Esther J. Mulyila na kushoto kwake ni Mhadhiri Mwandamizi** – UDSM, Bw. Paul Onyango akifuatiwa na Meneja Mkuu Mstaafu **TAFICO, Bw. Francis Nkoka. Kikao hicho kilifanyika jijini Dar es** Salaam Oktoba 1, 2020.



**Kaimu Meneja Mkuu TAFICO, Bi. Esther Mulyila (aliyesimama) akizungumza jambo wakati wa kikao cha kujadili vigezo mbalimbali vitakavyowezesha kupatikana mapendekezo ya aina ya vifaa vya uvuvi vya TAFICO vitakavyonunuliwa kupitia ufadhili wa Japan. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi, Bw. Emmanuel Bulayi akifuatiwa na Mhadhiri Mwandamizi – UDSM,** Bw. Paul Onyango. Kikao hicho kilifanyika jijini Dar es Salaam Oktoba 1, 2020.




**Picha ya pamoja ya washiriki wa kikao cha kujadili vigezo mbalimbali vitakavyowezesha kupatikana mapendekezo ya aina ya vifaa vya uvuvi vya TAFICO vitakavyonunuliwa kupitia ufadhili wa Japan kilichofanyika** Oktoba 1, 2020 jijini Dar es Salaam.

# SERIKALI YAGAWA INJINI ZA BOTI KWA VYAMA VYA WAVUVI KANDA YA ZIWA VICTORIA

Katika kuhakikisha shughuli za Wavuvi zinaboreshwa ili kukuza kipato chao, Serikali imegawa Injini za Boti nne (4) aina ya Yamaha zenye thamani ya shilingi milioni 35 kwa Vyama vya Ushirika vya Wavuvi vinne vinavyofanya shughuli zao katika Ukanda wa Ziwa Victoria.

Wakati akikabidhi Injini hizo kwa Wavuvi Wilayani Muleba Mkoani Kagera Oktoba 23, 2020, Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah alisema kuwa ugawaji wa Injini hizo ni katika kutekeleza moja ya majukumu ya Wizara ya kuhakikisha wanawezesha upatikanaji wa utaalamu, rasilimali fedha na vitendea kazi ili kuwasaidia Wavuvi kuboresha kazi zao na kuendeleza sekta ya uvuvi kwa ujumla.

Dkt. Tamatamah alisema kuwa katika kuhakikisha Vyama vya Wavuvi vinawezeshwa, mwaka wa fedha 2020/ 2021 Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetenga shilingi milioni mia mbili (200,000,000) kwa ajili ya kuviwezesha vyama vya Ushirika vya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe maji.

"Rai yangu kwa Vyama hivi vya Ushirika wazitumie injini hizi kwa kufanya uvuvi endelevu na kuachana na uvuvi haramu", alisema Dkt. Tamatamah

"Nawahamasisha pia wavuvi wajiunge katika vikundi vya ushirika ili iwe rahisi kuwezeshwa kwa mikopo na vitendea kazi ili waweze kujikwamua kiuchumi",aliongeza Dkt. Tamatamah.

Kuhusu mwitikio wa Wavuvi kujiunga na Vyama vya ushirika, Dkt. Tamatamah alisema kuwa mwitikio ni mzuri na Wilaya ya Muleba imekuwa kinara wa kuanzisha vyama hivyo.

Akiongea baada ya kupokea Injini ya Boti, Mwakilishi wa Chama cha Ushirika cha Wavuvi, Izigo, Wilayani Muleba, Naziru Kassanga alisema kuwa Injini hiyo ya boti waliyopatiwa itawasaidia sana wao kama wavuvi wadogo wadogo kufanya uvuvi wa kisasa utakaowasaidia kuboresha maisha yao.

"Injini hii itatusaidia sisi wavuvi wadogo kwenda kuvua katika kina kirefu kwa urahisi na kuondokana na uvuvi wa kienyeji ambao tija yake ni ndogo", alisema Kassanga

Naye, kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Wavuvi cha Zilagula,Wilayani Buchosa, Agnes Mbasha aliishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuwakabidhi boti ambayo anasema itawasaidia kufanya doria ya kulinda nyavu zao dhidi ya wezi.

"Nitumie nafasi hii pia kuwahamasisha wanawake wenzangu kujiunga na Vyama




**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (kulia) akikabidhi Injini ya Boti kwa Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Wavuvi, Zilagula, Agness Mbasha katika hafla fupi ya kugawa Injini za Boti kwa Vyama vya Ushirika vya Wavuvi Kanda ya Ziwa Victoria iliyofanyika katika Wilaya ya Muleba, Mkoani Kagera Oktoba 23, 2020.**



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi na Wawakilishi wa Vyama vya Ushirika vya Wavuvi Kanda ya Ziwa Victoria muda mfupi baada ya kukabidhi Injini za Boti kwa Vyama (4) vya Ushirika wa Wavuvi Oktoba 23, 2020. Kutoka kulia waliokaa ni Mkurugenzi Msaidizi, Huduma za Ugani za Uvuvi, Anthony Dadu na wa pili kutoka kulia ni Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani, Dkt. Erastus Mosha. Kutoka kushoto ni Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Omary Mchengule na wa pili kutoka kushoto ni Kaimu Mwenyekiti, Chama cha Ushirika cha Wavuvi, Zilagula, Agness Mbasha.**

hivi vya Ushirika kwani vinasaidia sana kujikwamua kimaisha",alisema Mbasha

Kuhusu Vyama vya Ushirika kuunganishwa na taasisi za fedha, Dkt. Tamatamah alisema mikopo iliyoombwa na kupitishwa kwa ajili ya vyama vya ushirika ni shilingi bilioni 2.6 na ambayo tayari imeshatolewa ni shilingi milioni 873.8 na vyama 14 viko katika hatua za mwisho kupatiwa mikopo.

"Wizara imeihamasisha Benki ya Posta Tanzania (TPB) kuzindua akaunti ya Wavuvi (Wavuvi account) kwa ajili ya mikopo na bima mahususi kwa Wavuvi hususani wavuvi wadogo", alifafanua Dkt. Tamatamah.




**Pichani ni Injini za Boti (4) aina ya Yamaha ambazo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imezikabidhi kwa Vyama vinne vya Ushirika vya Wavuvi Kanda ya Ziwa Victoria katika hafla fupi iliyofanyika Wilayani Muleba, Mkoani Kagera Oktoba 23, 2020.**



Jarida hili la Mtandaoni hutolewa kila mwezi na

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
**Wizara ya Mifugo na Uvuvi,**
S.L.P. 40487, Dodoma,Tanzania
Simu: +255763 255255
Email: www.mifugouvuvi.go.tz
Tovuti: www.mifugo.go.tz